# TAHARIRI

Makala za juzuu hili la 18 zinahusu mada mbalimbali kuhusiana na lugha, fasihi na utamaduni wa Kiswahili na lugha za Kiafrika. Makala ya Chebet-Choge inachunguza kuenea na kuendelea kwa lugha ya Kiswahili kuanzia kitovuni mwake katika mwambao mwa pwani ya Afrika Mashariki ambamo Kiswahili kilitumika kama lugha asilia na jamii ya Waswahili hadi kufikia hadhi yake ya sasa ya kimataifa. Makala inabainisha sababu mbalimbali ambazo zimeeneza Kiswahili tangu nchi za Afrika Mashariki zilipopata uhuru hadi kufika kiwango cha kimataifa hivi leo. Kwa upande wake, makala ya Msigwa inachunguza mwingiliano na uamilifu wake katika kujifunza lugha ya pili na jinsi ya kukuza mwingiliano huo katika mazingira ya kujifunzia lugha husika. Kwa kuchunguza wanafunzi wa shahada ya umahiri wanaojifunza Kiswahili nchini Rwanda, makala imebaini kwamba mwingiliano una nafasi kubwa na ya pekee katika kumpatia mjifunzaji lugha ingizotambuzi. Aidha, imebaini kuwa mwingiliano unaleta matokeo chanya katika maendeleo ya lugha ya pili.

Naye Vincent anachunguza dosari zinazofanywa na wajifunzaji wa Kiswahili katika jamii ya Wairaki nchini Tanzania ambao wanajifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili na kutathmini dosari zinazojitokeza kwa kiwango cha juu zaidi zikilinganishwa na dosari nyingine. Mwandishi amebaini kwamba dosari za upatanisho wa kisarufi ndizo hufanywa kwa kiwango cha juu kwa wajifunzaji hao. Sababu kadhaa za kujitokeza kwa dosari hizo zimebainishwa. Naye Jjingo katika makala yake anazungumzia ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni na lugha ya pili rasmi nchini Uganda. Makala inahimiza kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili na kuwa na sera imara ya lugha hiyo nchini humo. Kwa kulinganisha *Sera ya Utamaduni* ya Tanzania na Sera ya Taifa ya Utamaduni ya Uganda, mwandishi anapendekeza wapangaji lugha wa Uganda wajifunze na kuzingatia mambo kadhaa kutoka *Sera ya Utamaduni* ya Tanzania wakati wa upitiaji wa sera yake ya lugha.

Makala ya Sultan inachunguza utamaduni mahuluti kupitia mhusika Kehinde katika riwaya ya *Kehinde* (Emecheta, 1994). Mwandishi wa makala anaonesha namna Emecheta anavyotumia imani ya *chi* (mungu binafsi na roho) kutoka jamii ya Igbo kusawiri utamaduni, utambulisho, maisha na hatima ya Kehinde kama mhusika mwanamke Mwafrika kutoka jamii ya Igbo lakini anayeishi ughaibuni. Lugha ni kipengele muhimu katika kazi za fasihi. Sinzore, Amukowa na Ambuyo wanachunguza mitindo ya lugha inayotumiwa na wanawake viongozi na wahusika wengine katika tamthilia za *Pango* (2003) na *Kigogo* (2016) inavyojenga taswira ya kiongozi mwanamke. Makala imebaini taswira mbalimbali za mwanamke kupitia mitindo hiyo ya lugha. Makala ya Mwendwa, Ngugi na Ndungo inachunguza aina za vielelezo vilivyotumika katika usilimishwaji wa hadithi ya

*Wasifu wa Mwana Kupona* (King'ei, 2008) kutoka *Utenzi wa Mwana Kupona* (1972) na *Alisi Ndani ya Nchi ya Ajabu* (Hadjivayanis, 2015) kutoka *Alice's Adventure in Wonderland* (Carrol, 2011) na mchango wake katika kuendeleza ujumbe. Makala imebaini na kueleza dhima kadhaa za vielelezo vilivyotumika kwenye matini hizo.

Makala ya Mahenge inachambua dhima mbalimbali za msimulizi zinazotumika kusimulia hadithi ya ualbino katika bunilizi ya watoto iitwayo *Zindera* (2008). Kupitia Nadharia ya Naratolojia mwandishi amebaini msimulizi ana dhima kadhaa katika bunilizi hiyo. Aidha, imebainika kwamba msimulizi wa kazi hii anasawiri mitazamo miwili iliyopo katika jamii kuhusu watu wenye ualbino, mtazamo wa kizamani na mtazamo wa kisasa. Makala ya Sosoo inachunguza jinsi safari ya msako ya shujaa wa ngano za jamii ya Waewe kutoka Ghana na riwaya ya *Kufikirika* kutoka Tanzania inavyobeba vipengele vya utamaduni na falsafa ya Kiafrika. Kwa kutumia ruwaza ya shujaa ya Campbell (1973) makala imebaini kuwa kuna vipengele mbalimbali vya utamaduni na falsafa ya Kiafrika vinavyobebwa na ushujaa unaosawiriwa katika motifu ya safari ya msako katika matini teule.

Naye Sanga anachunguza namna utandawazi ulivyoleta mkengeuko wa ujumi wa Kiafrika wa hadithi fupi andishi za Kiswahili kutoka zile za asili ambazo ni hadithi fupi simulizi. Makala imebainisha athari kadhaa, chanya na hasi kwa kumakinikia vipengele mbalimbali. Masuala ya mabadiliko katika tanzu za fasihi simulizi yanachunguzwa katika makala ya Samwel. Mwandishi anarejelea tanzu kadha na kubaini mabadiliko yake kifani, kimaudhui, kiutendaji na kiuhifadhi. Makala pia inaeleza sababu kadhaa zinazotokana na mabadiliko hayo na mustakabali wa fasihi hiyo.

Sanga amechunguza mbolezi za sasa za jamii ya Wakinga wa mkoani Njombe zinazotendwa msibani ili kubaini dhima zake. Kwa kutumia Nadharia ya Ontolojia ya Kibantu, makala imebaini kwamba mbolezi hazina dhima tu ya kuliwaza kama tafiti nyingi zinavyodai bali zina dhima mbalimbali katika jamii hiyo.

**Wahariri, 2020**